REVELATION

UFUNUO

na

Rev. J. P. Hughes

Chapishwa na:
United Pentecostal
Church of Tanzania
SLP 1271, Moshi

UTANGULIZI

1. MLINGANISHO WA KITABU CHA MWANZO NA UFUNUO

A. Dhambi ilianzia Mwanzo, na mwisho ikashughulikiwa katika Ufunuo.

B. Shetani alianza shughuli zake katika Mwanzo - matokeo ya shughuli zake zinaonyeshwa katika Ufunuo.

C. Anguko la mwanadamu limeandikwa katika kitabu cha Mwanzo - kurejeshwa kwake kikamilifu kunaonekana katika Ufunuo

D. Ruhusa ya kuukaribia Mti wa Uzima yapotea katika Mwanzo - katika Ufunuo inarejeshwa tena.

2. TAFSIRI YA ELIMU NNE ZA KITABU CHA UFUNUO

A. **Elimu ya Yaliyopita.** Elimu hii inadhaniwa kuanzishwa na Jesuit Alcasari katika mwaka 1613 B.K. Inadai kwamba Ufunuo ulitimizwa kwa kuanguka kwa Yerusalemu na dhiki ya upagani katika siku za awali za Kanisa

B. **Elimu ya Kiroho.** Elimu hii inaamini kwamba Ufunuo inafafanua mapambano kati ya Kristo na Shetani - jema na ubaya.

C. **Elimu ya Historia.** Elimu hii inasisitiza kwamba kitabu cha Ufunuo ni ukamilifu wa Historia ya Kanisa la Kikristo, na kwamba matukio yalikuwa yameendea kutimizwa. Sehemu kubwa ambayo imekwisha tekelezwa tangu wakati wa Kristo.

D. **Elimu ya Wakati Ujao.** Elimu hii inashikilia kwamba Ufunuo bado ni wakati ujao, nayo kuwa ni sura tatu za awali. Wanashughulika na maono ya Kristo (sura ya 1), na kanisa la wakati uliopo (sura 2 & 3). Tutajifunza Ufunuo kutoka katika sehemu hii ya elimu ya wakati ujao. Inaonekana kuwa na maana sana katika kujifunza hoja yenye uhakika wa tofauti zote za mawazo ya tafsiri.

3. KIINI KATIKA TAFSIRI YA KITABU CHA UFUNUO

A. Moja ya maswali makubwa yanayopitia katika njia za wanafunzi wa Ufunuo ni, “Jinsi gani nitatafsiri mambo ninayokutana nayo katika kitabu hiki?” Mtu asiyeangalia swali hili kwa udadisi, kuwaza kwa akili ya kielimu, na kiroho bila shaka itaishia kwenye mawazo potofu. Kitabu chenyewe kinatoa kiini cha tafsiri katika Ufunuo 1:19. Aya hii inaonyesha kuwa kuna
MIGAWANYO MITATU YA KITABU.

1. **Mgawanyo wa Kwanza.** “Mambo hayo uliyoyaona”
    a) Maono ya Kristo - 1:12-19
    b) Mifano ya maono yatafsiriwa - 1:20
2. **Mgawanyo wa Pili.** “Mambo yatakayo kuwepo”
    a) Makanisa saba ya Asia - 2:1 hadi 3:22
    b) Muhula uliopo wa Kanisa, pamoja na nyakati zake tofauti, ambazo makanisa saba yanawakilisha kwa uwazi.
3. **Mgawanyo wa Tatu**. “Yale yatakayokuwa baada ya hayo”
    a) Hema ya ki-mbinguni na watakatifu walionyakuliwa pamoja na Bwana. Sura ya 4 & 5.

b) Kipindi cha Dhiki ambacho ni JUMA LA 70 LA DANIELI. Sura 6-19. Utaona uwiano mkubwa na unabii wa Danieli katika sehemu hii.
c) Ufunuo 19:11-20:15. Sehemu hii inaonyesha kuja kwa Yesu mara ya pili; kufungwa kwa Shetani; miaka elfu moja ya utawala Kristo na watakatifu Wake duniani; sehemu ya shughuli za Shetani katika utawala wa Kristo na hukumu; na Kiti cha Enzi Kikubwa cheupe cha hukumu.
d) Ufunuo 22:1-22:7. Katika sehemu hizi tunapata tazamo la mara moja katika umilele na kuona "mambo mapya".
e) Ufunuo 22:8-21. Tamati ya Kitabu.

SURA YA KWANZA

1. SALAAM: Zinaanza na aya ya 4

A. **"Kwake Yeye Aliyeko"** - Hii inamwonyesha kama Kuhani wetu Mkuu. Ni vizuri sana kufahamu kuwa YEYE YUKO siyo Yeye Alikuwako.
   1. Kutoka 3:14-16. MIMI NIKO AMBAYE NIKO
   2. Waebrania 4:14, 15. Tunaye kuhani mkuu
   3. Waebrania 7:25, 26. "…Maana Yu hai siku zote ili awaombee. …Tuwe na kuhani mkuu namna hii…"

B. **"Aliyekuwako"** Hii inamwonyesha Yesu kama Nabii.
   1. Kumbukumbu 18:15. Bwana atawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako…"
   2. Luka 24:19. "Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda mema na kunena mbele za Mungu."

C. **"Na Atakayekuja"** Hii inamwonyesha Kristo kama Mfalme.
   1. 1 Timotheo 6:15 "…Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana…"
   2. Ufunuo 19:16 pamoja na Danieli 2:34.

D. "**Kutoka kwa ROHO SABA walioko mbele ya Kiti Chake ya Enzi"**
   1. Yohana 4:24; Waefeso 4:4; 2 Wakorintho 3:17; yote yanafundisha kuwa Mungu ni Roho MOJA. Kwa hivyo namba saba haizungumzii idadi ya Roho bali katika "ukamilifu na utimilifu" wa Roho Mmoja.
   2. Isaya 11:2 inaonyesha matamshi saba ya pamoja ya utimilifu mmoja wa Roho.
      a. BWANA, HEKIMA, UFAHAMU, SHAURI, UWEZA, MAARIFA, KUMCHA BWANA.

E. **"Kutoka kwa Yesu Kristo"** aya ya 5.
   1. **Shahidi mwaminifu.** Kazi iliyokwisha – Isa 55:4 & Yoh. 18:37
   2. **Limbuko la waliola.** Wakati uliopo- 1 Kor. 15:20-23; Kol. 1:15-18; Ebr. 7:16.
   3. **Mfalme wa wafalme wa dunia.** Zek. 14:9; 1 Tim. 6:15; Ufu. 19:16 angalia pia Dan. 4:25 & 7:14

2. UTUKUFU: Soma Wafilipi 2:9 & Isa. 12:4

A. **"Kwake Yeye Atupendaye"** Yoh. 3:16; Rum. 5:8, 9; 1 Yoh. 3:1

B. **"Kwa Yeye Atuoshaye"** Isa. 1:16; Mal. 3:5; Tito 3:5.

C. **"Ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu"** Ufu. 5:8

3. KIINI KIKUU CHA KITABU: aya ya 7

A. **Kuja kwa Yesu mara ya pili** ni kiini kikuu.

B. Kuja kwa Yesu mara ya pili kumetajwa:
1. Katika mwanzo wa kitabu, 1:7
2. Katikati ya kitabu, 11:15-18
3. Mwisho wa kitabu, 22:20

4. MAONO YA KRISTO: aya ya 12-18

A. Yesu anaonekana katikati ya vinara saba vya taa. Hii inamdhihirisha Yeye kama kuhani na hakimu pamoja. Kama kuhani, Huvivika vinara na kuvidumisha vikiwa vimejaa mafuta. Kama hakimu, Anaangalia juu ya mafundisho na hali ya kiroho za makanisa na hali ya kuwaleta watenda maovu kwenye hukumu.

B. **Hali nane za Kristo Katika Maono.**
1. Mwili wake ukiwa umefunikwa na vazi hadi miguuni.
2. Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu, nyeupe kama theluji. Angalia Dan. 7:9 sawa na Mzee wa Siku (hekima & umri).
3. Macho Yake yalikuwa kama ndimi za moto. Zab. 11:4 & Mithali 15:3
4. Miguu yake kama shaba iliyosuguliwa. Isa. 63:3 inazungumzia hukumu.
5. Sauti kama sauti ya maji mengi. Au ya umati wa watu.
6. Katika Mkono Wake wa kuume nyota saba. Aya 20. Anashikilia huduma.
7. Kutoka kinywani Mwake kunatoka upanga mkali ukatao-kuwili. Nguvu ya neno lake kuhukumu na kuangamiza. Ebr. 4:12.
8. Kuonekana kwake alikuwa kama jua ling'aalo katika nguvu zake. Kama "sehemu mng'ao" zilizozuiwa alioona Musa."

SURA YA PILI NA TATU
MAKANISA SABA

1. MAELEZO MATATU KWA PAMOJA NA MAKANISA SABA

A. **Maelezo ya Mahali.** Makanisa haya hasa ni yale yaliyokuwepo katika siku za Yohana. Kwenye Asia Ndogo.

B. **Maelezo ya Kiunabii.** Yanachambua vipindi saba au viwango vya historia ya kanisa kuanzia mwanzo hadi Unyakuo.

C. **Maelezo Binafsi.** Ina thamani kwa kila mmoja kupima pendo lao kwa nyaraka kwa haya makanisa Mtu anatakiwa aonyeke kwa makanisa yaliyoanguka na maonyo walioyapata. Vivyo hivyo mtu anatakiwa aimarishwe kwa mibaraka, ahadi, na Wasifu.

2. MPANGILIO WA NYARAKA ULITOLEWA

A. **Salaam:** Kila barua huanza na "Haya ndiyo anenayo." Baadaye inafuata moja ya hali ambazo kwa hizo Kristo alikuwa amedhihirishwa na Yohana katika sura ya kwanza. Angalia kwamba alidhihirishwa katika hali tofauti kwa kila kanisa. Kinachosemwa kuhusu Kristo kila mara kinalingana na kushindwa kwa Kanisa

B. **Wasifu:** Kila waraka ulikuwa na utambulisho wa kazi zilizofanywa, isipokuwa katika swala la Laodekia kanisa la mwisho,.

C. **Karipio:** Kufuatia wasifu, madhaifu ya kila kanisa yalitajwa na kukemewa, pamoja na tofauti na kanisa la Smirna (kanisa litesekalo) na Filadelfia.

D. **Maonyo:** Kila kanisa linaonywa kuhusu hukumu kama watashindwa kusikia, isipokuwa Smirna na Filadelfia.

E. **Ahadi:** Kila moja ya barua ilikuwa na ahadi kwa washindi, ambayo kwa kawaida inafanana na hitaji la Kanisa.

F. **Onyo la upole:** Kila kanisa lilipokea marudi yao hayo, "Yeye aliye na sikio alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa".

3. VIPINDI VYA KIUNABII.

A. **Efeso** lilikuwa kanisa la karne ya kwanza.

B. **Smirna** lilikuwa kanisa lilololeswa la karne ya 2 & 3.

C. **Pergamo** lilikuwa kanisa kutoka kati ya 312 hadi 500 B.K.

D. **Thiatira** lilikuwa kanisa la Kipindi cha Giza, hadi karne ya kumi na sita.

E. **Sardi** lilikuwa kanisa la Marejesho.

F. **Filadelfia** ni kanisa la mvua za mwisho za vuli na Kipindi cha Uamsho wa karne ya 19 & 20

G. **Laodikia** ni kanisa la wakati wa mwisho la ukafiri.

4. DONDOO MAALUM:

A. **Wanikolai** kikundi kilichotajwa katika sura ya 2:6, 15. Jina limetokana na maneno mawili, ya Kigiriki (nikao) na (laos)._Likiwa na maana "kutiisha watu". Ni mfano wa ukuhani ujao unaotawala watu. Angalia "Matendo" ya aya ya 6 inakuwa mafundisho katika aya ya 15. huku ikipingana na Math. 23:8.

B. **Siku Kumi za Dhiki** katika sura 2:10. Kanisa la kwanza lilipitia mateso makuu kumi.

1.	Nero	B.K.	64 - 68
2.	Domitiani	B. K.	95 - 96
3.	Trajani	B.K.	100 - 115
4.	Aurelius	B. K.	168 - 197

5.	Saverus	B. K.	203 - 210
6.	Maxmin	B. K.	235 - 237
7.	Decius	B. K.	250 - 253
8.	Valeriani	B. K.	257 - 260
9.	Aureliani	B. K.	276
10.	Deocletiani	B. K.	303 - 310

SURA YA NNE

KANISA MBINGUNI

Pamoja na sura ya 4 tunaingia katika mgawanyo wa kitabu cha Ufunuo; "Na Yale Yatakayo kuwa Baada ya Hayo", aya 1:19. Hii inaonekana wazi katika aya ya 1, inayoanza na BAADA YA HAYO na ina maelezo, "Nitakuonyesha mambo ambayo hayana budi kuwako BAADA YA HAYO." Kwa hivyo yaliyomo kwenye kitabu kuanzia sura ya nne na kuendelea yanachukua nafasi baada ya muhula wa kanisa hapa duniani.

1. (RAPTURE) KUTWALIWA KWA KANISA

A. Neno (Rapture) halionekani katika Biblia. Neno lenyewe lina maana, "furaha kuu au furahisha sana", na limetumiwa katika theologia kuelezea "Kutwaliwa kwa kanisa" atakako fanya Yesu mwisho wa muhula wa kanisa
   1. 1 Kor. 15:51:-58; "Angalia, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakini tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho…" Paulo anatushirikisha ufunuo wa kile kitakachotokea wakati Kristo atakaporudi kwa ajili ya Bibi Arusi.
   2. 1 Thes. 4:14-17; inaonyesha kwamba waamini wote wa Kanisa, pamoja waliokufa na walio hai, watatwaliwa kutoka duniani kwenda kumlaki Bwana mawinguni. Angalia sehemu ya maneno "Parapanda ya Mungu" ikilinganishwa na "Parapanda ya Mwisho" katika 1 Kor. 15:52.
   3. 1 Thes. 2:19; Unyakuo ndio tumaini letu, furaha yetu, na taji yetu ya furaha.
   4. Yak. 5:7, 8; "Kwa hiyo ndugu, vumilieni, hata kuja kwake Bwana"

B. **Unyakuo** utatokea kabla ya kipindi cha Dhiki Kuu.
   1. Lk 21:36; "Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate KUOKOKA KATIKA HAYA YOTE YATAKAYOTOKEA."
   2. Ufunuo 3:10; "Nami nitakulinda, utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote." Wakati huo bado haujawadia. Walakini utakapowadia kanisa LITAONDOLEWA, na HALITAKUWEMO.
   3. Kuanzia sura ya 3 na kuendelea neno KANISA halikutajwa.
   4. 2 Thes. 2:7; Yule mtu wa kuasi hawezi kuja sasa hadi nguvu ile izuiayo (Kanisa) itakopotwaliwa.

C. **Unyakuo** uonekanavyo katika Ufu. 4:1-3.
   1. **<u>Mlango ulikuwa umefunguliwa mbinguni</u>.** Kabla ya hapo mlango ulikuwa umefungwa. Mlango ulio wazi katika Ufu. 3:8 unaelezea wakati wa Uijnilisti.
   2. **<u>Sauti ya kwanza…sauti kama ya baragumu ikinena nami.</u>**
      a. Hii ilikuwa ni sauti ya Yesu Kristo. Linganisha Ufu. 1:10
      b. Angalia jinsi hii ilivyo sawa na 1 Thes. 4:16; na PARAPANDA YA MUNGU, PIA

1 Kor. 15:52; na PARAPANDA YA MWISHO ITALIA, MAANA PARAPANDA TALIA." Parapanda ya mwisho ya 1 Kor. 15:52 siyo sawa na ile ya 7 katika baragumu ya Ufu. 11:15 kwa sababu zifuatazo:

1) Katika unyakuo ni "baragumu ya Mungu". Baragumu ya Ufu. 11:15 ni "parapanda ya malaika wa saba".
2) Kwanza ni baragumu ya mbaraka. Baragumu nyingine ni ya **ole.**
3) Baragumu ya kwanza ni ya kuwakusanya watakatifu. Nyingine ni katikati ya juma baada ya Kanisa kuwa mbinguni.
4) Mtume Paulo hakuwa akijaribu kusema wakati halisi wa unyakuo katika 1 Kor. 15:52 na 1 Wathesalonike 4:16, bali inaonyesha uhakika ya tukio hili lijalo. Paulo alikuwa akifahamu vyema maandiko na hivyo alifahamu tarumbeta mbili za shaba katika Hesabu 10
   Tarumbeta hizi zilitumika kuita kusanyiko la Wana wa Israeli. kwa "parapanda ya mwisho" Paulo alikuwa anaelekeza kwa mwisho (mwito wa kusanyiko) utakaofanywa na Mungu Mwenyewe. 2 Wathesolonike 2:1, "…kukusanyika kwetu mbele zake".

D. **Ishara saba za Unyakuo Ujao**

1. **KITAIFA -** Math. 24:7; vita na matetesi ya vita
2. **KIMWILI** - Math. 24:7; matetemeko ya nchi, tauni, na njaa.
3. **KUHUSU BIASHARA** - Dan. 12:4; usafirishaji na maarifa.
4. **MAADILI** 2 Tim. 3:1-5; Lk 17:28; maadili yetu kama Sodoma.
5. **WAYAHUDI** Lk 21:29-31; Wayahudi wamerudi katika Nchi Takatifu.
6. **MAFUNDISHO** Math. 24:24: manabii wa uongo kuong ezeka
7. **KANISA** Math. 24:12; Ufu. 3:15, 16; wakati wa kukaza mwendo umewadia.

SURA YA NNE NA TANO

KUTAZAMA MBINGUNI

1. KATIKA SURA YA NNE, MUNGU ANAONEKANA NA KUABUDIWA KAMA MUUMBAJI NA KILA KITU KINAELEKEZWA KWAKE KUKIZUNGUKA KITI CHA ENZI.

A. Kiti cha enzi kilikuwa kimewekwa Mbinguni Na Mmoja na Kuketi Juu ya Kiti cha Enzi. aya 2
   1. Ebr 1:8; "Lakini kwa habari ya Mwana asema, kiti chako cha enzi, Mungu ni cha milele na milele…"
   2. Ufu. 3:21; "Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi."

B. **Mawe Matatu Yametajwa Katika Vifungu**. Rejea Kut. 28.
   1. **Sardi: Mawe 12** ya awali. Inasimama kwa ajili ya Reubeni. Jina Reubeni linamaanisha TAZAMA MWANA. Sardi ilikuwa na rangi ya wekundu- damu.
   2. **Yaspi: Jiwe la 12** la mwisho na husimama kwa ajili ya Benyamini. Benyamini maana yake MWANA WA MAMLAKA YANGU. Yaspi ilikuwa safi na kung'aa.
   3. **Zumaridi**: Zumaridi husimama kwa ajili ya Yuda. Yesu alikuwa SIMBA WA KABILA YA YUDA

C. **Wazee-Ishirini na Wanne. Uwakilishi wa KANISA**

1. Walikuwa wamepewa mataji na viti vya enzi. Ufu. 3:11, 21; 20:4.
2. Walikuwa wamevishwa kitani nzuri, ing'arayo. Ufu. 19:8.
3. Namba "ishirini na nne" inazungumzia "ukuhani". 1 Pet. 2:9 & 1 Nyak. 24:1-19. Makabila 12 kujumlisha Mitume 12.
4. Wanaimba wimbo wa ukombozi.

D. **Wanyama Wanne au Viumbe Hai**. Linganisha na Eze. 1
   1. Hawa ni makerubi hao hao wanaowakilisha vikosi vya mbinguni katika kumwabudu kwao Mungu. Aya ya 8
   2. Wanawakilisha mfano wa Kristo na Israeli.
      a) Simba - Yesu kama ilivyo katika Mathayo - Hesabu 2:3 Yuda
      b) Manadamu - Yesu kama ilivyo katika Luka - Hesabu 2:10 Reubeni
      c) Ndama - Yesu kama ilivyo katika Marko - Hesabu 2:18 Efraemu
      d) Tai - Yesu kama ilivyo katika Yohana - Hesabu 2:25 Dani.

E. **Swala la Kuabudu Ni Muumbaji.** Aya 11

2. KATIKA SURA YA TANO MUNGU ANAONEKANA NA KUABUDIWA KAMA MKOMBOZI NA MWANA KONDOO NI MTAZAMO HALISI

A. **Kitabu Chenye Mihuri Saba: aya ya 1**
   1. **Sehemu kitabu kilikokuwa:** Kilikuwa katika (mahali juu halisi) mkononi mwa muumbaji, aliyekuwa ameketi juu ya kiti cha enzi. KWA NINI MUUMBAJI HAKUSTAHILI KUKIFUNGUA KITABU?
   2. **Hali Ya Kitabu:**
      a. Kilikuwa kimetiwa muhuri na kingeweza kufunguliwa tu na anayestahili.
      b. Kilikuwa kinahusiana na dunia. Ile mihuri ilipofunguliwa, hukumu ilikuja DUNIANI. Hivyo ALIYEKUWA ANASTAHILI KUKIFUNGUA KILE KITABU ALITAKIWA AWE AMBAYE AMESHUGHULIKA ULIMWENGUNI. Lazima awe mwenye kukimiliki.
      c. Kiwe kinahusiana na ukombozi. Yesu alikuwa Mwokozi - Jamaa wa karibu aliyetwaa ulimwengu kwa Shetani.
   3. **Kukitwaa Kitabu:** Mwana-Kondoo alistahili kutwaa kitabu.

B. **Mwana-Kondoo**
   1. **Anaonekana kama Simba wa Kabila ya Yuda, Shina la Daudi.**
      a. Yesu kama Mungu ni Simba, lakini kama mwanadamu ni Mwana-Kondoo.
   2. **Alikuwa katikakati ya Kiti cha Enzi.**
      a. Aliyeko juu ya kiti cha enzi siyo tu Muumbaji, bali pia Mkombozi. Mwana Kondoo haimdhihirishe mwingine katika uungu, ila huonyesha WADHIFA WA UKOMBOZI
   3. **Kuonekana Kwake.**
      a. Pembe saba: pembe zinazungumzia mamlaka; Math. 28:18. Saba ni namba ya ukamilifu.
      b. Macho saba: hakuna kinachoepuka ufahamivu wa Roho wa Mungu. Zab. 11:4; 2 Nya. 16:9.
      c. Iliyotumwa ulimwenguni mwote: kutazama wema na kuubariki, kuutazama uovu na kuuleta hukumuni.

C. **Anaye-Abudiwa ni Mwana-Kondoo** (MKOMBOZI): aya 9

SURA YA SITA

DHIKI KUU

Dhiki Kuu itakuwa ni ghadhabu ya Mungu ulimwenguni. Itadumu kama miaka saba. Inawiana na unabii wa Danieli wa juma la mwisho la Danieli. Na itagawanyika katika sehemu mbili ya miaka mitatu na nusu. Sehemu ya kwanza inadhihirika katika sura ya 5 hadi 12, na sehemu ya mwisho inaonekana katika sura ya 13 hadi 19; Dan. 9:6; Ufu. 11:21; Ufu. 13:51.

Zab. 2:4, 5	Yer. 30:4-7
Dan. 12:1	Math. 24:21, 22
Ufu. 3:10	Ufu. 7:14

1. MIHURI SABA

A. **Muhuri wa kwanza**
1. Huyu ampandaye farasi mweupe ni MPINGA-KRISTO akianza shughuli zake mara baada ya unyakuo wa Kanisa.
2. Farasi mweupe ni ishara wa amani, ambayo itakuwa nimfumo wa Mpinga-Kristo mara atakapokuja mara ya kwanza. Dan. 8:25. Anaonyeshwa akiwa na upinde, lakini hauna mishale.

B. **Muhuri wa Pili**
1. Farasi mwekundu (rangi ya damu) na upanga mkononi mwa aliyempanda ni ishara ya vita.
2. Farasi mwekundu na aliyempanda inaonyesha maendeleo ya Mpinga-Kristo kupitia kuteka. Alama ya “amani ya uongo” inapewa nguvu kutoa amani ulimwenguni. Vita na ukiwa ni sehemu ya utawala wa Mpinga-Kristo. Dan. 9:26.

C. **Muhuri wa Tatu**
1. Farasi mweusi na aliyempanda ni ishara ya NJAA. Njaa ni matokeo ya kawaida ya Vita.
2. Dinari ilikuwa ni malipo ya kutwa. Math. 20:1-16. Hii inaonyesha chakula cha ghali kitakuja. Na kipimo cha ngano kilikuwa kama senti mbili katika Nyakati za Biblia, kilikuwa ni kibaba cha mateka. Thamani ya kawaida ilikuwa vipimo 8 kwa dinari.

D. **Muhuri wa Nne**
1. Aliyempanda farasi wa Kijivukijivu anaitwa MAUTI.
2. Kifo kinatakiwa kuja kwa njia ya upanga, wanyama wakali, njaa, na kwa kifo chenyewe.

E. **Muhuri wa Tano**
1. Roho chini ya madhabahu zilizochinjwa wakati ule wa ile mihuri minne. Utaratibu wote wa Mpinga-Kristo utakuwa ni kupinga Ukristo. Atashambulia watu wanomcha Mungu.
2. Waliouawa kwa sababu ya Neno la Mungu na ushuhuda walioushika.

F. **Muhuri wa Sita**
1. Kulikuwa na tetemeko kuu. Tetemeko la Matetemeko ya ardhi ni ya kawaida sana sasa na inaonekana kama yanaongezea. Angalia matetemeko matano (5) yaliyotajwa katika kitabu cha Ufunuo.
    a. Ufu. 6:12 - katika kufungua mhuri wa 6.
    b. Ufu. 8:5 - baada ya muhuri wa 7

c. Ufu. 11:13 - kufuatia kupaa kwa mashahidi wawili.
d. Ufu. 11:19 - baada ya baragumu ya 7
e. Ufu. 16:18 - katika kufunga kitasa cha 7

G. **Muhuri wa Saba**

1. Kulikuwa na UKIMYA mbinguni kama kipindi cha 1/2 saa. Ukimya huu lazima ulikwa katika agizo la ukimya wa utakatifu mbinguni. Hukumu za baragamu ya saba ziko tayari kuanza. Mungu aliamrisha muda wa kunyamaza katika kutazama ukali wa hukumu iliyokuwa haijaja bado.

2. BARAGUMU SABA

A. **Baragumu ya Kwanza**

1. Mvua ya mawe na moto vilivyochangamana na damu. Inaonekana kama mlipuko wa bomu la atomiki linalorusha maji hadi sehemu ya viwango vya juu mahali yanapoganda na kuanguka juu ya dunia kama mfano wa mawe ya barafu.
2. Mbaya kuliko mawe ya barafu yaliyoanguka juu ya Misri. Kutoka 9:24.

B. **Baragumu ya Pili.**

1. Kitu kama mlima uwakao moto ukatupwa baharini.
2. Theluthi moja ya bahari ikawa damu, theluthi moja ya viumbe hai baharini vikafa, na theluthi moja ya merikebu zikaharibiwa.

C. **Baragumu ya Tatu.**

1. Nyota kubwa ikaanguka juu ya theluthi moja ya maji safi. Nyota iitwayo pakanga.
2. Ilisababisha theluthi moja ya maji kuwa machungu, na matokeo yake wanadamu wengi wakafa.

D. **Baragumu ya Nne**

1. Theluthi moja ya mianga ikapapigwa.
2. Kupunguka kwa mwanga kutakuwa na matokeo ya maangamizi makuu kwa mazao, kupwa kwa maji/kujaa, hatari kwa usafiri wa angani na maji, na mifumo mingine ya maisha.

E. **Baragumu ya Tano**

1. Pigo la MATESO kwa kipindi cha miezi mitano.
2. Hakuna atakayeuawa kwa mateso haya.
3. Nzige ni mifano na siyo halisi, kwa sababu imetamkwa kuwa hawana mfalme. Mithali 30:27.
4. Hawatadhuru majani, vitu vibichi, au miti.
5. Nzige hawatadhuru watumishi wa Mungu 144,000.

F. **Baragumu la Sita**

1. Pigo ambalo theluthi moja ya wanadamu waliuawa.
2. Malaika wanne waliongoza jeshi la wapanda farasi wenye pepo 200,000,000.
3. Wapanda farasi waliuawa kwa matumizi ya moto, moshi, kiberiti.

G. **Baragumu ya Saba**

1. Kulikuweko na radi, sauti, ngurumo, mvua ya mawe, na tetemeko la nchi.
2. Sauti kutoka mbinguni zilitangaza mambo kadhaa vitakavyotokea kipindi hiki.
3. Mataifa yalighadhibika kwa ghadhabu ya Mungu iliyokuja.

4. Sanduku la Agano lilionekana kwenye hekalu la Mungu.
5. Tarumbeta ya 7 inaweka alama ya kati ya miaka saba.

3. VITASA SABA (gudulia): sura ya 16

A. **Kitasa cha Kwanza**
   1. Majipu mabaya (yanayouma) juu ya wale wenye Alama ya Mpiga Kristo.

B. **Kitasa cha Pili**
   1. Sehemu zote za maji ya chumvi zikageuka kuwa damu.
   2. Kila kitu katika maji ya chumvi kilikufa.

C. **Kitasa cha Tatu**
   1. Vyanzo vyote vya maji vikageuka damu.
   2. Sawa na moja ya pigo ya Misri. Kut. 7:17-21.

D. **Kitasa cha 4.**
   1. Miale ya jua ikapewa kuwaunguza kwa moto.
   2. Ukanda wa unaozuia miale ukaathirika.
   3. Wanadamu bado hawakutubu.

E. **Kitasa cha 5**
   1. Ulimwengu ulitumbukizwa katika giza kuu.
      a. Wanadamu wakatafuna ndimi zao kwa sababu ya giza.
      b. Wanadamu wakaendelea kumkufukuru Mungu kwa sababu ya maumivu yao.
      c. Sawa sawa na moja ya mapigo ya Misri. Kut. 10:21

F. **Kitasa cha 6**.
   1. Mto Frati wakauka na kufanyika njia kuu.
      a. Wafalme watokao katika mashariki ya jua wataitumia ile njia. Isaya 11:15-16

G. **Kitasa cha 7**.
   1. Kinamiminwa juu ya anga.
      a. Kinaleta sauti kuu, radi, ngurumo, matetemeko ya nchi.
      b. Babeli inagawanywa katika sehemu tatu.
      c. Milima na Visiwa vyote havikuonekana.
      d. Mvua ya mawe yenye uzito wa kilo 50 yakaanguka juu ya nchi.

SURA YA SABA

WAISIRAELI 144,000 WATIWA MUHURI

1. HAWA NI KINA NANI?

A. Waisraeli waliotiwa mhuri - Ufu. 7:1-8
   1. 12,000 kutoka kila kabila
   2. Kabila la Lawi lachukua mahali pa kabila la Dani.
      a. Dani lilikuwa kabila la kwanza kuabudu sanamu. Waamuzi 18.

b. Dani waliacha urithi wao wa asili. Waamuzi 18:1
c. Moja ya sanamu za ndama za Yeroboamu aliiweka huko Dani. 1 Fal. 12:29.

3. Kabila la Efraemu liliitwa Yusufu (baba yake Efraemu).

B. Waliitwa "WATUMISHI WA MUNGU WETU"
1. Walikataa kuungana na majeshi ya Mpinga-Kristo.
a. Katika siku za Eliya 7,000 walikataa kumtumikia Baali.

C. Wanaokombolewa kutoka ulimwenguni. Ufu. 14:3
1. Wanao uchaguzi kuwa katika hiyo idadi.
2. Wanaonekana kama kuwakilisha makabila kumi na mbili kwenye Kiti cha Enzi.

D. Inarejelea kwa MTOTO-MWANAMUME katika. Ufu. 12:5.
1. Wale 144,000 wanaoneka mbinguni katika sura ya 14.

2. MAMBO TUNAYOFAHAMU KUHUSU WALE 144,000.

A. Kama ilivyorekodiwa katika Ufunuo.
1. Waliimba wimbo ambao hakuna aliyeweza kuimba wimbo ule, Ufu. 14:3
2. Hawakutiwa unajisi na wanawake, 14:4
3. Kwa maana ni bikira, 14:4
4. Walimfuata Mwana-Kondoo kila Aendako, 14:4
5. Wanaitwa "malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo", 14:4
6. Haukuonekana uovu kwenye midomo yao, 14:5
7. Mbele ya kiti cha enzi haukuonekana na uovu, 14:5
8. Walikuwa na jina la Baba yao limeandikwa juu ya vipaji vya nyuso, 14:1
9. Watatiwa muhuri katikati ya muhuri wa 6 & 7, na hatadhurika na baragumu ya hukumu, 7:3
10. Watanyakuliwa kama ilivyo Mtoto-Mwanamume, sura ya 12

3. SABABU KWA NINI 144,000 SIYO KANISA

A. Kanisa litakuwa kutoka kila Taifa, siyo Israeli tu.

B. Kanisa ni Bibi Arusi na siyo Watumishi.

C. Kanisa Siyo Tu Kwa Mabikira.

D. Kanisa linatiwa muhuri na Roho Mtakatifu, na Siyo kwa Malaika.

E. Kanisa halitakuwa ulimwenguni baada ya sura ya 3.

4. UMATI MKUBWA AMBAO HAPANA MTU AWEZAYE KUUHESABU: UFU. 7:9-17

A. Ni tofauti Kutoka wale 144,000.
1. Mkutano mkubwa hauhesabiki kutoka kila taifa, jamaa, kabila.

B. Wao ni tofauti Kutoka katika Kanisa.

KANISA	MKUTANO USIOHESABIKA
1. Mataji	1. Hakuna mataji
2. Kukaa katika viti vya enzi kuzunguka Kiti cha Enzi cha Mungu	2. Kusimama mbele ya Kiti cha Enzi
3. Vinubi na Vitasa (vyetezo) mikononi mwao.	3. Matawi ya mitende
4. Wafalme na makuhani	4. Hakuna lililotamkwa
5. Kutawala ulimwenguni	5. Wakitumika mchana na usiku

SURA YA KUMI NA MOJA

MASHAHIDI WAWILI

1. UTAMBULISHO WA MASHAHIDI WAWILI

A. Wao ni Manabii Wawili. Ufu. 11:3, 6, & 10.

B. Wao ni WAPAKWA MAFUTA. Zek. 4:14.

C. Wanaingia katika Kielelezo cha Musa na Eliya.
   1. Kuondoka kwao ulimwenguni ni MUUJIZA.
      a. Mwili wa Musa ulifichwa na Mungu. Kumb. 34:6 & Yuda 9
      b. Eliya alitwaliwa na Mungu. 2 Wafalme 2:11.
      c. Wote wawili walikuwa mlimani Yesu alipogeuka sura. Lk 9:30, 31
   2. Musa aligeuza Maji Kuwa Damu. Kut. 7:20.
   3. Eliya alifunga Mbingu kwa Miaka 3 $^{1}/_{2.}$ Yak. 5:17.
   4. Ilikuwa imetabiriwa Kwa Eliya kuwa atarudi. Mal. 4:5, 6.

2. HUDUMA YAO ULIMWENGUNI ITAKUWA LINI?

A. Watahudumu kwa Siku 1,260, miaka 3 ^{½}

B. Itakuwa kati ya Miaka 3 $^{1}/_{2}$ ya Dhiki.
   1. Walinyakuliwa mwishoni mwa Ole ya 2 ambayo ni sawa na Baragumu la 6. Ufu. 9:12, 13 & Ufu. 11:12-14.

3. NI NINI HUDUMA YA HAO MASHAHIDI WAWILI?

A. Wanafanya Kazi Ya Nabii.
   1. Kutangulia kusema matukio yajayo.
   2. Kulia dhidi ya dhambi ya wakati.
   3. Kulinda dhidi ya mafundisho ya uongo.

B. Wanayo nguvu ya kuuwa kwa moto utokao vinywani mwao. Aya 5

C. Wanaweza kuzuia mvua na kuita mapigo yashuke. Aya 6.

D. Watauawa na Mpinga-Kristo. Aya 7

E. Watachukuliwa kupelekwa Yerusalemu kwa ajili ya maonyesho. Aya 8

F. Watafufuliwa kutoka katika wafu baada ya siku 3 1/2. Aya 11, 12

G. Kusudi la Huduma Yao.
   1. Kuwashawishi Wayahudi kuhusu Umasihi wa Yesu.
      a. Wanawakilisha SHERIA & MANABII.
      b. Eliya kugeuza mioyo ya watoto kuelekea baba zao. Mal. 4:5,6 & Lk 1:17
      c. Kuiunganisha imani ya Wayahudi kwa wazee wao. Lk 8:56
   2. Wayahudi humtumia Musa na Eliya kuunganisha kupitia wao kwa wao MUNGU MMOJA.

SURA KUMI NA MBILI

MSHANGAO MKUU MBINGUNI

1. MWANAMKE: Aya 1 & 2

A. Mwanamke ni Mfano wa Taifa la Israeli: Isa. 54:5-8
   1. Mwanamke siyo KANISA, kwa kuwa Kanisa limezungumziwa kama bikira safi, na siyo mwanamke.
   2. Siyo Bikira Maria, kabisa Mariamu hakuwahi kufichwa nyikani kwa miaka $3^1/_2$.

B. Jua, Mwezi, na Nyota zinazungumzia juu ya Mfumo wa Sola (Sola System). (Israeli katika utukufu wa jua, utatawala kote siku moja kupitia Ufalme wa Mwana wa Daudi).
   1. Nyota 12 inaelezea Makabila Kumi na Mbili ya Yakobo
   2. Linganisha ndoto ya Yusufu katika Mwa. 37:9.

C. Israel kuona uchungu katika kuzaliwa. Isa. 9:6; 66:7-10; Mik. 5:2, 3.

D. Israeli kuadhibiwa. Yer. 30:11

2. JOKA KUBWA JEKUNDU: Aya- 3, 4, 9

A. Joka ni Shetani - aya ya 9
   1. Vichwa Saba inazunguzia ukamilifu wa hekima: Eze. 28:12
   2. Pembe Kumi inazungumzia nguvu kubwa.
   3. Mkia, unaokokota theluthi mbili ya nyota, inazungumzia malaika walio na ushawishi wa kuungana naye. Aya 9.

B. Kazi zake Ovu
   1. Anasimama mbele ya mwanamke kumdhuru mtoto wa yule mwanamke mara tu azaliwapo. Aya 2
   2. Yeye na malaika wake walikuwa kinyume na Mikaeli na malaika wake. Aya 7
   3. Alitupwa ulimwenguni na kumwudhi yule mwanamke. Aya 13
   4. Akafanya vita dhidi ya masalia ya uzao wa yule mwanamke. 17

3. MTOTO MWANAMUME: Aya 5

A. Isa. 66:7, 8; inaonyesha yule mtoto mwanamume ataokolewa kabla ya maumivu na uchungu. Wakati wa "kipindi cha taabu ya mwanamke" ni katika kipindi cha mwisho wa mwisho wa miaka 3 ½ ya dhiki.

B. Dan. 12:1; "Wakati huo Mikaeli atasimama, jemedari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa TAABU, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; NA WAKATI HUO WATU WAKO WATAOKOLEWA; Kla mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile."

C. Mtoto Mwanamume inawakilisha wale Waisreli 144,000 waliotiwa muhuri, ambao awali wametajwa katika sura ya 7, na baadaye katika sura ya 14 wakionekana mbinguni. Kutwaliwa kwa yule Mtoto Mwanamume kwa hivyo inaweza kukurejewa kwa kutwaliwa kwa 144,000 kwa kuwa hakuna kutajwa kwingine kuhusiana nayo.
   1. Wale 144,000 wana hali zinazofanana na Kristo.
      a. Wote wanaume
      b. Mabikira
      c. Malimbuko ya kwanza 1 Kor. 15:23
      d. Hana ila 1 Pet. 2:22
      e. Hakuwa na hatia Yoh. 19:6

4. MAHALI PA MAFICHO: Aya 11-16

A. **JANGWANI** inafanana na mahali Israeli walipowekwa kwa miaka 40 Alipoondoka Misri. Hos. 2:14, 15

B. MOABU & EDOMU KUEPUKA KUTOKA Mpinga-Kristo. Dan. 11:41
   1. Isa. 16:1-5; "…waliofukuzwa waache wakae pamoja nawe, Moabu."
   2. Mji PETRA katika Edomu ni ngome ya kawaida.

5. MABAKI: Aya 17

A. Zek. 13:8, 9, inadhihirisha theluthi moja tu ya Israeli itaepuka Mpinga-Kristo.

B. Mabaki watakubali Kristo kuwa Masihi, bila shaka ikiwa ni matokeo ya huduma ya Mashahidi Wawili.

SURA YA KUMI NA TATU

WANYAMA WAWILI

1. WANYAMA KUTOKA BAHARINI

A. Kuja Kwake Kumetangulia Kutamkwa.
   1. Danieli alimwona kama PEMBE NDOGO: Dan. 7:8, 24-28; 8:9-14, 21
   2. Danieli alimwona kama MNYAMA; Ufu. 13:1-7; 17:7-17
   3. Paulo alimwona kama MTU WA KUASI; 2 Thes. 2:3-8

B. Majina mengine Ambayo Anayoitwa
   1. Agano la Kale

a. Ashuru; Isa. 10:5, 6; 14:24, 25; 30:27-33
b. Mbaya; Isa. 11:4
c. Mfalme wa Babeli; Isa. 14:4
d. Lusiferi; Isa. 14:12
e. Mfalme wa Tiro; Eze. 28:11-19
f. Pembe Ndogo; Dan. 7:8; 8:9-12
g. Mfalme mwenye Uso Mkali; Dan. 8:23
h. Mkuu Atakayekuja; Dan. 9:26
i. Mfalme Afanyaye Atakavyo Dan. 11:36

2. Katika Agano la Jipya.
a. Mtu wa Kuasi; 2 Thes. 2:3-8
b. Mwana wa Uharibifu; 2 Thes. 2:3-8
c. Yule Asi; 2 Thes. 2:8
d. Mpinga-Kristo; 1 Yoh. 2:18
e. Mnyama; Ufu. 13:1-8

C. Tabia za Yule Mnyama
1. Vichwa Saba
a. Vichwa 7 ni vilima saba (falme); Ufu. 17:10
b. Tano kati ya hizo zilianguka siku za Yohana; Ufu. 17:10, Misri, Ashuru, Babeli, Uamedi-Uajemi, na Ugiriki.
c. Ya 6 ilikuwa ni Roma, iliyokuwa inatawala katika siku za Yohana
d. Ya 7 bado haijaja.
Ya saba ni sawa na miguu ya chuma iliyochanganyika na udongo katika ile sanamu inayoonekana katika Danieli sura ya pili (2).
2. Pembe Kumi
a. Pembe 10 ni wafalme 10 watakaotawala na kichwa cha 7, na kumpa mamlaka yeye. Ufu. 19:12
3. Kuonekana kwake kama Chui, Dubu, & Simba, rejea Dan. 7
4. Nguvu zake zinatoka kwa Joka
a. Shetani alimwambia Yesu kuwa atampa. falme za dunia. Math. 4.
b. Mamlaka kudumu kwa miezi 42. Ufu. 13:5
c. Malaika kuenea ulimwengu mzima. Ufu. 13:7
d. Mamlaka kufanya vita na Mwanakondoo na watakatifu Wake. Ufu. 11:14
5. Atauawa na kufufuliwa. Ufu. 13:3
a. Kuigiza kama Kristo halisi.
b. Atadai kuwa Mungu. Dan. 11:36, 37; 2 Thes. 2:4
c. Atakuwa sehemu ya Myahudi kafiri. Dan. 11:37
6. Mwisho wake utakuwa ziwa la moto. Ufu. 19:20
a. Anaonekana kwenye ziwa la moto zaidi ya miaka 1,000. Ufu. 20:10

2. MNYAMA KUTOKA KATIKA NCHI

A. Pia huitwa **NABII WA UONGO**. Ufu. 19:20
1. Ni wa tatu katika utatu usio mtakatifu.
2. Mbili ya pembe za kondoo zinamdhihirisha kuwa mbwa mwitu katika mavazi ya kondoo, kwa kweli ni nabii wa uongo
3. Sauti ya yule joka inaonyesha uwezo wake wa kuzungumza. Kama Haruni alivyokuwa msemaji wa Musa, atakuwa msemaji wa Mpinga-Kristo.

B. Utendaji Wake
1. Kujificha katika ushawishi wa biashara

a. Kuanzisha Alama ya yule Mnyama; Ufu. 13:16
b. Hakuna atakaye nunua wala kuuza pasipokuwa na alama.

2. Ushawishi wake juu ya dini
   a. Kusababisha ulimwengu wote umwabudu Mpinga-Kristo. Aya 12
   b. Kutengeneza sanamu ya Mpinga-Kristo. Aya 14
   c. Kufanya sanamu kuwa hai. Aya 15
   d. Kusababisha wote wasioiabudu ile sanamu kuuawa. Aya 15
3. Anaishia pia kwenye ziwa la moto. Ufu. 19:20

SURA YA KUMI NA SABA NA KUMI NA NANE

BABELI

1. BABELI YA KIMWILI

A. Mwanzo wake.
1. Ilianza kama BABELI na mwanzilishi wake akiwa Nimrodi. Mwa. 10:10
2. Mungu alishuka kuwatawanya watu kwa kuchafua lugha yao. Mwa. 11
3. Kulingana na historia, Babeli palikuwa mahali pa kwanza kuabudu miungu ya uongo.

B. Ufalme wa Nebukadneza - kama mwaka 600 K.K.
1. Ilitumiwa na Mungu kuadhibu ufalme wa Yuda. 2 Wafalme 20
2. Ilitawala ulimwengu. Dan. 2:37, 38
3. Mahali pa kuabudu sanamu. Dan. 3:1
4. Uliangushwa na Dario Mmedi. Dan. 5:31

C. Baada ya kuangushwa na Utawala wa Uamedi - Uajemi
1. Ulifanyika mji mkuu katika Utawala wa Uajemi. Dan. 6:1
2. Ulitembelewa na Alexandra Mkuu, na hapo ndipo alipofia.
3. Petro aliandika waraka wake wa kwanza akiwa Babeli. 1 Pet. 5:13
4. Sasa ni mji wa HILALI, ukiwa na maelfu kadhaa ya watu.
5. Unabii wa Isaya (Isa. 1:19, 20) lazima bado ni wakati ujao.

2. BABELI YA KIDINI

A. Kahaba Mkuu - Ufu. 17
1. Analo jina limeandikwa kwenye kipaji cha uso, “SIRI BABELI MKUU, MAMA MKUU WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA YA NCHI.”
2. Mwanamke ni mji ukaao juu ya vilima saba, unaotawala juu ya falme za dunia. Ufu. 17:9, 18
   a. Wafalme wa dunia wanafanya uzinzi na huyo mwanamke.
   b. Amelewa damu za watakatifu na wafia dini.
   c. Anaonekana kama tajiri sana.
   d. Anaonyeshwa akiwa <u>amekaa juu ya mnyama</u>. Au yuko katika mashirikiano na Mpinga-Kristo.
   e. Ataangamizwa na wafuasi wa Mpinga-Kristo.
3. Kwa hivyo tuna hitimisha kwamba mwanamke ni maendelezo ya “mfumo wa dini ya uongo” iliyoanzishwa Babeli, na hata falme zote kwa karne nyingi. Katika nyakati za mwisho atafungamana na Mpinga-Kristo ili tu asiangamizwe naye.

3. BABELI YA KISIASA

A. Mnyama wa Rangi ya Zambarao.
   1. Yule mnyama ni mwanadamu. Ufu. 13:18
   2. Rejea kama vile mfalme wa Babeli katika unabii. Isa. 14
   3. Mpinga-Kristo atafanyika mtawala katika utawala uliohuishwa wa Rumi, (sanamu ya Danieli ya miguu ya chuma na udongo).
   4. Ili kuvuta kuabudiwa mwenyewe, ataondoa mifumo yote ya kidini. Ufu. 13

4. MLINGANISHO WA AGANO LA KALE & JIPYA

A. Yer. 50:13 na Ufu. 18:4 - mapigo ya Babeli.

B. Yer. 50:15 na Ufu. 18:6 - “kama alivotenda yeye, mtendeni yeye”

C. Yer. 50:19, 20 aya hizi zinaeleze kuanguka kwa Babeli wakati ujao katika siku za Dan. Kwa hivyo lazima ziendane na Ufu. 18

D. Yer. 50:23 na Ufu. 18:19 - kuharibiwa kwa Babeli.

E. Yer. 50:25 na Ufu. 16:19 - linganisha silaha za Mungu na vitasa.

F. Yer. 50:29 na Ufu. 17:16 - linganisha wapiga mishale na wale wafalme 10

G. Yer. 50:46 na Ufu. 18:9 - kilio kilisikika katika mataifa

H. Yer. 51:6 na Ufu. 18:4 - toka kati ya watu wake

I. Yer. 51:8 na Ufu. 18:10 - katika lisaa limoja

J. Yer. 51:48 na Ufu. 18:20 - furaha mbinguni juu ya lile anguko.

SURA YA KUMI NA TISA

VITA VYA ARMAGEDONIA

1. VITA VYA ARMAGEDONIA NI NINI?

A. Armagedonia (urefu ya Megiddo) ni sehemu katika ukanda wa Yezreeli kati ya Mlima Karmeli na Mlima Tabori, kama maili 60 kaskazini mwa Yerusalemu.

B. Hapo vita vitapiganwa kati ya Mpinga -Kristo na majeshi ya Yesu na majeshi ya mbimguni. Aya 11-19

2. KUSUDI LA VITA

A. Ni tendo la hukumu ya Mungu dhidi ya majeshi ya Shetani katika kumalizia Dhiki Kuu.
   1. Isa. 24:21 - kuwaadhibu walio na nyadhifa za juu & wafalme wa ulimwengu.

2. Isa. 26:21 - kuwaadhibu wakaao juu ya nchi.
3. Isa. 34:2 - kuangamiza majeshi yote ya mataifa
4. Isa. 63:6 - kushusha chini nguvu (uhai wa damu) wa mwanandamu.
5. Isa. 66:19 - kutangaza utukufu wa Mungu katika mataifa
6. Eze. 38:20- kuharibu kazi ya mwanadamu (kila ukuta)

3. MAHALI PA VITA

A. Katika eneo la maili 176 urefu kaskazini na kusini mwa Yerusalemu. Kutoka ukanda wa Esdraeloni kaskazini mwa Edomu na kusini.

1.	Ufu. 16:16	Har-Magedoni
2.	Yoeli 3:13	Bonde la Yehoshafati
3.	Zek. 12:2, 3	Yersalemu na Yuda
4.	Zek. 14:2, 3	Yerusalemu
5.	Isa. 34:5	Edomu
6.	Isa 63:1	Edomu na Bosra
7.	Oba. 15	Edomu

4. MATOKEO YA VITA

A. Juu ya majeshi ya Mpinga-Kristo
1. Kina cha damu kitakuwa mpaka kwenye hatamu ya farasi na kusambaa maili 176 urefu. Ufu. 14:20
2. Karamu ya ndege warukao. Ufu. 19:17, 18; Eze. 39:17
3. Mpinga-Kristo na nabii wa uongo watupwa kwenye ziwa la moto. Ufu. 19:20
4. Kuzika maiti itachukua miezi 7. Eze. 39:12
5. Kusafisha mabaki ya silaha itachukua miaka 7. Eze. 39:9

B. Katika Ulimwengu kwa Ujumla
1. Waliouawa kuonekana ulimwengu wote. Yer. 25:33
2. Mataifa yote kuletwa katika hukumu. Yoeli 3; Math. 25
3. Ulimwengu wote kuteketezwa kwa moto wa wivu wa Bwana. Sef. 3:8

C. Nchi halisi
1. Mlima wa Mzeituni kugawanyika, na mto mpya utatokeza kati ya Bahari ya Mediterenian na Bahari ya Chumvi; Zek. 14:4-8; Eze. 47:1-12
2. Kila kilima kuanguka na kila kisiwa kuzama; Ufu. 16:16-20

D. Wayahudi kumkubali Yesu Kama Masihi; Zek. 12:9; 13:7

5. MADHARA YA VITA VYA ATOMIKI YANAONEKANA KATIKA HAR-MAGEDONIA

A. Mabonge ya barafu ya uzito wa kilo 50 kuanguka. Ufu. 16:21
1. Mabonge makubwa ya barafu yalipatikana wakati majaribio ya chini ya maji yakifanyika huko Bikini mwaka 1946.

B. Watu wa Japani waliteseka kwa jambo lilo hilo linaloelezewa katika Zek. 14:12 wakati walipodondoshewa bomu la atomoki.

C. Majeshi ya Mpinga-Kristo yataangamizwa na Yesu kwa "…mng'ao wa kuja kwake." 2 Thes. 2:8

SURA YA ISHIRINI

UTAWALA WA YESU WA MIAKA 1000

1. UFAFANUZI

A. Kitakuwa ni kipindi katika historia ya mwanadamu cha miaka 1,000 ya amani, chini utawala wa kimbinguni wa Yesu Kristo. Yeye akiwa wa uzao wa Daudi, atatawala kutokea Yerusalemu.

B. Wakati wa utawala wa miaka 1000 ahadi zote zilizoahidiwa kwa Ibrahim zitatimizwa.

C. Utawala wa miaka 1000 utaanza mara baada ya Vita Har-Magedonia.

2. KUSUDI LA UTAWALA WA MIAKA 1,000

A. Itakuwa ni jaribio la mwanadamu kutoka kwa Mungu. Wanadamu watakuwa wakichunguzwa kuhusu tabia chini ya hali ya maadili.
   1. Atashindwa kama nyakati nyingi; Ufu. 20:7-9

B. Itakuwa ni ushuhuda jinsi ambavyo ungekuwepo kama isingekuwa ni ushawishi wa Shetani. Ufu. 20:1-3

3. UTAWALA WAKATI WA UTAWALA WA MIAKA 1,000

A. Kutakuweko na serikali ya **THEOKRASIA.** (kutawaliwa na Mtawala Mkuu mmoja) Yesu Kristo.
   1. Yesu Masihi atakuwa mfalme. Isa. 9:3-11; Lk 1:32

B. Kanisa Kushiriki Utawala kupitia Kristo.
   1. Kanisa litatawala ulimwenguni. Ufu. 5:10
   2. Waaminifu kuwa wakuu wa miji. Lk 19:17

C. Israeli
   1. Watainuliwa juu ya Mataifa Isa. 14:1, 2
   2. Watakuwa makuhani wa Mungu. Isa. 61:6
   3. Mitume 12 watakuwa wakuu wa Israeli. Math. 19:28

D. Mataifa ya Mataifa (wasio wa-Israeli)
   1. Hukumu ya Mataifa katika Mathayo 25 itaamua ni taifa gani katika Mataifa yatakuwepo katika utawala wa miaka 1,000.
   2. Mataifa yote yatatakiwa kwenda Yerusalemu kuabudu. Zek. 14:16-21

4. DINI KATIKA KIPINDI CHA UTAWALA WA MIAKA 1,000

A. Wokovu Utakuja Kwa Wote. Isa. 55:1-3
   1. Sawa na tukio la Kuzaliwa Mara ya Pili. Eze. 36:25-27

B. Ibada za Hekalu kurejeshwa. Eze. 40:1 hadi 46:24
   1. Hekalu kutoa mahali pa Kiti cha Enzi. Eze. 43:7
   2. Mahali pa kuendelezea dhabihu za Kumbukumbu.

a. Siyo dhabihu za kuondoa dhambi. Ebr. 10:4
b. Kuwa Kumbukukumbu kama ilivyo Meza ya Bwana kwetu leo.

5. MABADILIKO KATIKA NCHI NA AINA YA MAISHA YA WATU NA WANYAMA

A. Nchi
1. Palestina itakuwa ukanda wenye rutuba; Eze. 47:1-12
2. Palestina itagawanywa kwa Mkabila 12; Eze. 48

B. Maisha kwa Ujumla
1. Wanyama watakuwa wapole. Isa. 11:6-9
2. Hakuna magonjwa. Isa. 33:24; Eze. 34:16
3. Urefu wa maisha utarejeshwa. Isa 65:20
4. Mfanikio kiuchumi. Isa. 65:21-23; Yoe. 2:21-27
5. Maarifa kwa wote. Isa. 11:9; Isa. 54:13
6. Lugha moja. Sef. 3:9
7. Hakuna vita. Mik. 4:3; Isa. 32:17, 18

SURA YA ISHIRINI NA MOJA NA ISHIRINI NA MBILI

WAKATI WA UMILELE

1. KWA WALIOPOTEA

A. Kiti Cha Enzi Cheupe cha Hukumu
1. Hukumu kulingana na matendo yao. Ufu. 20:13; Rum. 6:23
   a. Kutakuwepo na viwango vya adhabu. Lk 12:47, 48
2. Kuhukumiwa kwa kutokuwa na majina yao kwenye Kitabu cha Uzima. Aya 15

B. Mauti ya Pili
1. Moto wa milele. Math. 25:41
2. Mahali pa mateso. Lk 16:28; Ufu. 14:11
3. Ziwa liwakalo moto na kiberiti. Ufu. 21:8
4. Hakuna kupumzika mchana na usiku. Ufu. 14:11
5. Mahali pa kilio na kusaga meno. Math.8:12
6. Weusi wa giza kwa milele. Yuda 13
7. Funza wao hawafi. Mk. 9:44
8. Hakuna kuepuka. “Bonde kubwa limewekwa”. Lk 16:26

2. KWA WALIOOKOLEWA

A. Mbingu Mpya (mji mtakatifu uitwao Yerusalemu Mpya)
1. Ukubwa wa mji
   a. 12,000 “furlongs” (2,219.25 kilomita au maili 1,500) Mraba kwenda juu
   b. Kuta kuwa 144 mraba (futi 216) kwenda juu
2. Uhakika wa Mji
   a. Kuta zikiwa na misingi 12 za mawe ya thamani.
   b. Barabara za dhahabu safi kama kioo.

c. Mto wa uzima ukibubujika kutoka humo.
d. Ndani yake hakuna hekalu.
e. Mwana-Kondoo wa Mungu ndiye chimbuko la nuru.
f. Una milango 12 ambayo kamwe haifungwi iliotengenezwa kwa lulu.
g. Kichafu hakiruhusiwi pale.

3. Maisha katika mji
   a. Maisha ya ushirika na Yesu. Ufu. 22:4
   b. Mahali pa mapumziko. Ufu. 14:3
   c. Maarifa kamili. 1 Kor. 13:12
   d. Hakuna machozi. Ufu. 21:4
   e. Hakuna mauti. Ufu. 21:4
   f. Hakuna magonjwa. Ufu. 22:2
   g. Maisha ya kumwabudu Mungu. Ufu. 19:1

B. Nchi Mpya
   1. Itajawa na watu wenye haki. 2 Pet. 3:13
   2. Hakutakuweko na bahari tena. Ufu. 21:1
   3. Utaangazwa na mji mtakatifu. Ufu. 21:24
   4. Itakuwa na wafalme na mataifa. Ufu. 21:24.